**HOTUBA YA MHESHIMIWA DKT. SAMIA SULUHU HASSAN, RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, KUPOKEA SHAHADA YA UDAKTARI WA HESHIMA KATIKA UONGOZI [HONORARY DOCTORATE (*HONORIS CAUSA) IN LEADERSHIP]* YA CHUO KIKUU MZUMBE - MOROGOTO TAREHE 24 NOVEMBA, 2024**

- *Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Mkuu wa Chuo, na Rais Mstaafu wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi;*
- *Mheshimiwa Prof. Adolph Mkenda (Mb.), Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia;*
- *Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu Mawaziri Mliopo;*
- *Balozi Dkt. Emmanuel Nchimbi, Katibu Mkuu wa Chama cha Mapinduzi;*
- *Mheshimiwa Adam Kighoma Malima, Mkuu wa Mkoa wa Morogoro;*
- *Ndugu Makatibu Wakuu na Manaibu Makatibu Wakuu Mliopo;*
- *Wakuu wa Vyombo vya Ulinzi na Usalama*
- *Prof. Saida Yahya-Othman, Mwenyekiti wa Baraza la Chuo;*
- *Wajumbe wa Baraza la Chuo Kikuu Mzumbe;*
- *Prof. William Mwegoha, Makamu Mkuu wa Chuo;*
- *Prof. Allen Mushi na Prof. Eliza Mwakasangula, Manaibu wa Makamu Mkuu wa Chuo;*
- *Viongozi na Wafanyakazi wote wa Chuo Kikuu Mzumbe;*
- *Waheshimiwa Wageni Waalikwa;*
- *Wahitimu wenzangu wa leo;*
- *Wana Mzumbe wote na Wananchi wote mlioko hapa;*
- *Mabibi na Mabwana.*

**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!**

**Chuo Kikuu Mzumbe!**

Nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema ya uhai na kutuwezesha kushiriki tukio hili. Nalishukuru pia Baraza la Chuo Kikuu Mzumbe kwa uamuzi wake wa kunipa heshima ya kunitunuku Shahada ya Udaktari wa Heshima katika Uongozi (*The Honorary Doctorate (Honoris Causa) in Leadership*) ya Chuo Kikuu Mzumbe. Nafarijika kwamba shahada hii leo inatolewa na Chuo kilichonijengea misingi ya kuwa kiongozi katika Taifa hili.

Aidha, ninafuraha kusema kwamba, pamoja na shahada niliyopokea leo, namshukuru Mungu kwamba nimekwishatunukiwa shahada nyingine tano (5) za udakatari wa heshima kutoka vyuo mbalimbali nchini na duniani. Nimepokea kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu cha Jawaharlal Nehru cha India, Chuo Kikuu cha Sayansi za Siasa cha Uturuki, Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar, na Chuo Kikuu cha Anga cha Korea. Hii ni shahada ya tano (5), nami nimesimama hapa kwa unyenyekevu mkubwa, kukubali heshima hii ninayopewa na Chuo Kikuu cha Mzumbe Morogoro. ***Ahsanteni sana!***

***Mheshimiwa Mkuu wa Chuo***, kutambuliwa na Chuo chenye historia ya kuwa tanuri la kuoka viongozi wa Taifa hili, ni heshima kubwa sana. Najisikia fakhari kwamba Chuo kilichonijenga na kunitayarisha kuwa kiongozi kimetambua kazi yangu na leo hii kinanitunuku shahada ya heshima. Kwa kuwa suala la uongozi lina mchango wa watu mbalimbali, naitoa Shahada hii ya heshima kama zawadi kwa wote wenye mchango kwenye maisha yangu ya kiuongozi, akiwemo Mkuu wa Chuo hiki Rais Mstaafu wa Zanzibar, Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein, ambaye ni mmoja wa walionifanya kuwa nilivyo leo. Lakini pia naitoa Shahada hii kwa wananchi wote wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Kwa kuwa niko na wahitimu wenzangu hapa, nitumie fursa hii pia kuwapongeza kwa dhati kwa jitihada zenu kitaaluma na kwa kuweka historia ya kuhitimu pamoja na Mkuu wa Nchi, ambaye historia yake ya kitaaluma imejengwa katika Chuo hiki, wakati huo kikijulikana kama Institute of Development Management

(IDM), Mzumbe. Ni matumaini yangu kwamba, sitakuwa mhitimu wa mwisho kutoka Chuo hiki kukabidhiwa dhamana ya kuiongoza nchi yetu, bali atapatikana mwana Mzumbe mwingine, awe kati yenu wahitimu wenzangu wa leo, au waliotutangulia na hata wajao, atakayebeba dhamana ya kuliongoza Taifa letu.

***Mheshimiwa Mkuu wa Chuo***, nchi yetu imetimiza zaidi ya miongo sita ya kujitawala. Mimi, ni Rais wa sita katika kuitumikia nchi hii. Baada ya Baba wa Taifa aliyefanya kazi kubwa ya ukombozi na kuweka misingi madhubuti ya kuendesha Taifa letu, alifuatiwa na viongozi mahiri ambao, katika vipindi vya uongozi wao, walitoa mchango mkubwa, na kila mmoja kumuachia anayemfuatia, misingi imara ya kuendeleza Taifa letu kisiasa, kiuchumi na kijamii. Kila Awamu ya uongozi ilikuwa na mchango uliyoiwezesha Taifa letu kuwa lenye utawala bora, utulivu wa kisiasa na uchumi unaoeleweka kwa nyakati husika. Vilevile, wameendeleza Taifa lenye amani na mshikamano. Kwa nyakati tofauti, viongozi walionitangulia, walilazimika kushughulikia masuala waliyoyakuta kabla wao, wakashughulikia yaliyojitokeza wakati wao na kuweka misingi kwa yanayoweza kutokea baada ya awamu zao. Ndio kusema kwamba, ***kiongozi ni mtumishi anayeendeleza ya jana, akabuni, kuibua na kutekeleza ya leo; na akaacha ya kuendelezwa kwa ajili ya kesho.***

Kama ilivyokuwa kwa watangulizi wangu, Awamu hii ya sita nayo imekumbana na changamoto za kukabiliana na mazingira iliyoyarithi, kutatua changamoto zilizoibuka katika kipindi hiki, na bila shaka itaweka misingi kwa ajili ya Awamu zijazo.

***Mheshimiwa Mkuu wa Chuo,*** kwa ufupi nataka kuyaangalia mapito ya safari yangu katika uongozi hadi hapa nilipofika. Mengi yamekwishasemwa hapa, lakini niseme maeneo yote niliyopita yamenijenga kiwezo na yalinifungulia upeo wa maarifa na kuweza kufanya mengi ambayo kwa sasa hivi tunaendelea kuyatekeleza. Hapa

ninakusudia kubainisha mambo ambayo nilikabiliana nayo na yakanikuza kiakili na kuufungua zaidi upeo wangu wa maarifa.

Mosi; vurugu za kisiasa zilizotokea Zanzibar mwaka 2001 na kuleta mtafaruku mkubwa uliogharimu maisha ya wananchi wenzetu. Pamoja na kuwa nilikuwa mpya kwenye ulingo wa kisiasa, niliaminiwa kuwa mmoja wa Mawaziri waliopewa jukumu la kuieleza jumuiya ya kimataifa kilichotokea, na hatua zinazopangwa kuchukuliwa kuituliza nchi na kurudisha amani. Katika kufanya kazi hii nilikuwa na Dkt Shein, akiwa Waziri wa Katiba na Utawala Bora wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, na mimi nikiwa Waziri wa Kazi, Vijana, Ajira, Maendeleo ya Wanawake, na Watoto. Kazi hiyo ilimalizika kwa kupata muafaka wa kuendesha Serikali ya Umoja wa Kitaifa, ambayo ndiyo suluhu ya kisiasa kwa Zanzibar hadi leo.

Jambo la Pili; uwepo wa Bunge la Katiba mwaka 2014 ambapo nilihudumu kama Makamu Mwenyekiti wa Bunge hilo, nikimsaidia Hayati Samwel Sitta, aliyekuwa tayari na uzoefu mkubwa wa kusimamia mijadala mikali Bungeni. Ikiwa ni mara ya kwanza nchi yetu kuunda Bunge la Katiba lenye uwakilishi mpana wa aina ile, nililazimika kusimamia vikao vilivyojumuisha mchanganyiko wa watu wenye uzoefu, weledi na makuzi tofauti. Pamoja na kwamba baadhi ya vyama vya siasa vilisusia mchakato ule tukiwa tunafikia ukiongoni mwa kazi tuliyopewa, tulifanikiwa kuandika Katiba inayopendekezwa. Zoezi hili nalo lilikuwa na mafunzo mengi na makubwa ya namna ya kufanya kazi na makundi yenye malengo na mirengo tofauti ya Kisiasa.

Pamoja na mapito hayo, hakuna uzoefu ambao ungeweza kuniandaa kwa taarifa ya kumpoteza Rais aliye madarakani, Hayati John Pombe Magufuli. hili lilikuwa ni tukio kubwa na la kufadhaisha. Nilikabidhiwa dhamana ya Rais, Mkuu wa Nchi na Amiri Jeshi Mkuu katika kipindi ambacho Taifa kwa mara ya kwanza limeondokewa na Rais aliyeko madarakani, na nikiwa Rais wa kwanza nchini mwenye jinsia ya kike, mambo ambayo kwa miongo 6 ya uhai wa Taifa letu, haikuwahi kufikiriwa, na haikuwahi kutokea.

Pamoja na hali hiyo, dunia pia ilikuwa ikikabiliwa na changamoto kubwa ya UVIKO-19 ambayo mbali na vifo vya watu wengi, janga hilo lilisababisha athari kubwa za kuporomoka kwa uchumi duniani. Nikiwa bado najipanga *kukubaliana* na uhalisia wa kuwa Mkuu wa Nchi na *kukabiliana* na changamoto zinazoambatana na dhamana hiyo, ikazuka vita ya Urusi na Ukraine ambayo ikichanganywa na UVIKO-19 ilizorotesha sana mnyororo wa usambazaji wa bidhaa mbalimbali duniani, ikiwemo bidhaa muhimu kwetu kama vile ngano, mbolea na vipuri vya viwandani. Wakati hayo yakiendelea, mabadiliko ya sera za kifedha huko Marekani yakaleta athari kwenye upatikanaji wa Dola ya Marekani ambayo ni sarafu kuu katika biashara za kimataifa. Mambo yote hayo yakitokea ndani ya miaka mitatu ya awali ya awamu hii ya sita, na papohapo nchi yetu ikiwa inatekeleza miradi mikubwa ya kitaifa iliyohitaji fedha nyingi sana.

Nilidhani niyaeleze hayo ili tupate hali halisi niliyoanza nayo. Zipo nadharia mbalimbali kuhusu uongozi, wapo wanaosema kwamba, kiongozi huzaliwa na karama ya uogozi, wapo wengine wanasema viongozi hutengenezwa. Si dhamira yangu kujiingiza kwenye mjadala wa nadharia hizo. Ninachoweza kusema kwa uhakika ni kwamba, ***baharia mzuri hujulikana wakati wa dhoruba, sio wakati bahari ikiwa shwari.***

***Mheshimiwa Mkuu wa Chuo***, unaweza ***kuwa kiongozi*** hata kwa miaka 20 lakini ukapata ***nafasi chache za kuongoza***. Nafasi ya kuongoza, ikimaanishwa kudhihirisha kipawa cha uongozi na kuwavusha unaowaongoza katika changamoto inayohitaji utatuzi. Ninamshukuru Mungu kwamba, mapito ya safari yangu katika nyadhifa mbali mbali za uongozi, yamenipa maarifa ya kuweza kuwaongoza wenzangu katika kulitumikia Taifa hili, na ninafarijika kwamba, Mungu ameendelea kutuonesha njia ya kupita, mimi na wenzangu tulioko Serikalini. Naweza kusema kuwa mtindo wangu wa uongozi umejengeka juu ya misingi mikuu mitatu, ambayo ni **ushirikishaji**; **kutumia**

**ushahidi katika maamuzi (*evidence-based decisions)*;** na **kutanguliza maslahi ya Taifa.**

***Mheshimiwa Mkuu wa Chuo***, nikianza na ushirikishwaji, pengine umewahi kusikia nikitamka kauli kwamba, *nchi hii ni ya Watanzania wote*, na kwamba, *kila Mtanzania ana haki ya kuchangia katika ujenzi wa Taifa letu*. Kwa kuzingatia uzoefu nilioupata kutokana na hali ya kisiasa Zanzibar, hususan uendeshaji wa Serikali ya Umoja wa Kitaifa, nilipokabidhiwa dhamana ya kuwa Rais, niliiona haja ya kuwaunganisha Watanzania ili wote turudishe hisia za utaifa na tuishi kama watu wa Taifa moja. Ndiyo maana mimi na wenzangu tulikuja na Falsafa ya R4 (yaani Maridhiano (Reconciliation), Mabadiliko (Reforms), Ustahimilivu (Resilience) na Kujenga Upya (Rebuilding)) ambayo Profesa Mwenegoha ameielezea vizuri sana. Niliamini na bado ninaamini kwamba, kuzungumza na kupata muafaka wa namna ya kuendesha mambo yetu, na kustahamiliana, kuvumiliana kutaleta utulivu mkubwa utakaotuwezesha kufanya kazi zetu na kuwahudumia wananchi kwa salama na amani, na kuwa na maendeleo endelevu.

Katika msingi huu wa ushirikishaji, ndani ya kipindi cha Awamu hii, tumefanya uamuzi wa kuirejesha Tume ya Mipango, ili tuweze kupanga kwa pamoja na kuwa na uratibu mzuri zaidi wa mipango yetu. Pamoja na kurejesha Tume hiyo na kuiwezesha kiutendaji, tumefanya pia uamuzi wa kutunga Sheria ambayo, pamoja na mambo mengine, inataka mipango yote ya Serikali, ya muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu lazima ijadiliwe na kuridhiwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ni katika jitihada za kushirikishana, nikitambua kwamba Bunge ndio linawakilisha wananchi wa Jamhuri hii.

***Mheshimiwa Mkuu wa Chuo***, jambo la pili ni uamuzi unaozingatia ushahidi. Msingi mwingine unaotuongoza katika kufanya mageuzi na kuendesha shughuli za Serikali, ni **maamuzi yanayozingatia ushahidi** yaani ***evidence-based decision making*.** Kikubwa hapa ni masuala ya Ufuatiliaji na Tathmini (*Evaluation and Monitoring*). Ili

kupata maridhiano, tumeunda kamati, vikosi kazi na Tume kadhaa za kutafiti jinsi ya kuendesha shughuli mbalimbali za kiserikali zinazohusu haki za raia, mahusiano ya kidiplomasia, udhibiti wa uchumi, uendeshaji wa taasisi na mashirika ya Umma, tafiti za mageuzi ya sera kama ilivyoelezwa vizuri kuhusu sekta ya elimu, uandishi wa Dira ya Taifa 2050 na kadhalika. Katika mambo yote haya, tulifanya utafiti, tukapata maoni ya watu, tukapata ushauri wa kitaalam na ndio tukafanya maamuzi. Maamuzi ya Serikali hufanyika baada ya kupata maoni ya wananchi, na ushauri wa kitaalamu na wenye ushahidi wa mambo.

Hata hivyo, wakati mwengine, watu hutaka kuona ushahidi kwa kiongozi kuonesha njia. Na mfano mzuri kwenye hili ni baada ya kupata janga la UVIKO 19, tulikuwa na mjadala mzito kuhusu watu wachanje au wasichanje. Na kama Mkuu wa Nchi nilipotoka na kuchanja hadharani na watu waliponiona waliofuata njia na kuchanja, na tukaweza kudhibiti maradhi haya.

Kwa ujumla, msingi wa uamuzi unaozingatia ushahidi, unatufanya tuwe na uelewa wa pamoja, kwani maamuzi yanayotokana na ushahidi wa kisayansi yana uwezo zaidi wa kujibu kwa weledi matatizo na mahitaji yetu.

***Mheshimiwa Mkuu wa Chuo***, jambo la tatu, ni kuzingatia maslahi ya Taifa ni msingi mwingine unaotuongoza na ndiyo moyo wa uzalendo. Uamuzi wowote tunaoufanya kwa nchi yetu, pamoja na kupata ushauri kuhusu jambo husika, na baada ya kupata ushahidi wa kutosha, kipimo cha mwisho ni je, jambo hili lina maslahi kwa Taifa? Na, je, suala hili lina maslahi kwa Watanzania?

Na hapa, ninarudi kulekule kwenye UVIKO-19. Tulipopata janga lile, dunia ilipata fursa ya kupata fedha za mkopo nafuu sana. Lakini fedha zile zilitolewa na mashirika makubwa ya fedha ili tununue chanjo, tununue barakoa, na tununue vitakasa mikono. Kwa ufupi ilikuwa fedha ya mkopo tuirudishe ili wakubwa wafanye biashara. Lakini kwa upande wetu, tuliona lile halina maslahi kwa Taifa.

Tafsiri yetu ya kupambana na UVIKO-19 ilikuwa kupunguza wanafunzi madarasani. Madarasa yetu yalikuwa na wanafunzi 120 tukasema tupunguze angalau darasa liwe na wanafunzi 50. Na ndipo tulipojenga madarasa 12,000 ya shule za msingi. Tukajenga pia ya shule za sekondari na shule za awali (*early childhood education).* Tukasema pia ili kupambana na UVIKO-19, lazima wananchi wawe na vituo vya kutolea huduma za afya katika maeneo yao. Yakitokea majanga wananchi wahudumiwe kule badala ya kukimbizwa katika hospitali za Wilaya na Mikoa. Ndipo tulipojenga vituo vya afya katika Kata na zahanati katika maeneo mengine. Tatu, tulisema kukabiliana na UVIKO-19 ni kuwa na maji safi. Kwa mwaka moja tulipata fedha kueneza maji safi na salama ndani ya nchi. Kwetu sisi, kwa uongozi wetu, tuliona hayo yana maslahi makubwa zaidi kwa Taifa.

Kuzingatia maslahi ya umma ni pamoja na kutoa kipaumbele kwa maeneo yanayougusa umma. Zaidi ya nusu ya Watanzania wanategemea sekta kadhaa, ikiwemo elimu, afya, umeme na kilimo, na huko ndiko tunakopeleka nguvu kubwa ya Serikali. Kwa mfano, katika sekta ya kilimo, bajeti ya sekta hiyo imepanda kutoka **Shilingi bilioni 519** mwaka 2020/2021 hadi **Shilingi trilioni 1.49** mwaka 2024/2025. Tumepeleka fedha nyingi tukijua kwamba kilimo ndio ajira za vijana, kilimo ndio usalama wa chakula, kupitia kilimo tunatengeneza biashara baina ya nchi zetu za Afrika. Tunapeleka umeme vijijini kutengeneza pia ajira kwa vijana, na vijana wautumia kujiari kwenye mambo mbalimbali. Huduma za afya na za elimu, zote zinaenda kugusa umma.

Ninachoweza kusisitiza kuhusu uongozi iwe katika ngazi ya familia, kwenye asasi za kiraia, biashara au uongozi wa kisiasa, ni kwamba uongozi ni lazime utoke moyoni, na ushajihishwe na maadili (ethics) na uadilifu (integrity). Ukiwa na hivyo vitatu, na la nne, baraka za Mwenyezi Mungu, utaona mambo yanakwenda. Kiongozi afanye uamuzi sahihi hata kama hakuna mtu anayemfuatilia. Atende au kutokutenda kwa kusukumwa na nafsi safi na dhamira njema kwa kuzingatia maslahi ya Taifa.

Ukisema hili jambo halifai kufanywa nafsi yako na dhamira njema ikusukume hivyo. Na ukisema hili nikilifanya litaleta matumaini na litaleta faida kwa watu, nafsi yako na dhamira yako ikusukume kufanya hivyo. Na hivyo, unaweza sasa ukawa kiongozi wa watu.

***Mheshimiwa Mkuu wa Chuo*;** niruhusu nimpongeze Makamu Mkuu wa Chuo kwa hotuba yake ya kina kuhusu mwenendo wa Chuo hiki. Ninamshukuru kwa maneno mazuri kwangu na kwa Serikali ninayoiongoza. Ninamshukuru pia Prof Binamungu, ambaye amefanya utafiti wa kutosha. Nilipata taarifa kwamba chuo hiki kinataka kunituniku, niliuliza jambo kubwa linalowasukuma kunipatia heshima hii. Kile nilicholetewa na kusoma ni nusu ya yaliyoelezwa leo hapa na Prof. Binamungu.

Nimesikiliza kwa makini, mipango na ubunifu wa Menejimenti katika kutekeleza miradi mbalimbali, ikiwemo matumizi ya vyanzo vya ndani. Na hili limenifurahisha sana. Ninampongeza Mkuu wa Chuo, kwa kazi kubwa ambayo yeye na wenzake, wanaendelea kufanya hapa Mzumbe.

Nimevutiwa zaidi na utaratibu wa ***crowdfunding*** ambao unaendana na msingi mmojawapo wa uongozi wangu, yaani ushirikishwaji. ***Crowdfunding*** inatoa fursa ya kuonesha uongozi kupitia dhana pana ya uongozi niliyoifafanua hapo mwanzo. Ni vizuri kila mhitimu wa Mzumbe, akaona fahari kuwa sehemu ya mafanikio ya Taasisi hii iliyomfanya awe alivyo leo, kwa kuitikia wito wa Chuo. Tujisikie fahari.

Ninataka kuwaambia kwamba wakati mimi ninaingia hapa mwaka 1983, hali haikuwa hivi hata kidogo. Ninakumbuka siku ya kwanza nimefika chuoni hapa, nikapelekwa Matola ambalo lilikuwepo bweni langu kuanzia mwaka wa kwanza hadi wa mwisho. Mzumbe hii ilikuwa huoni kitu, ni milima na misitu. Usiku unaona tu macho ya simba. Kwa sisi tuliotoka pwani na kuvuka maji ilikuwa shida kwelikweli. Unajiuliza 'ikitokea shida hapa ninakimbilia wapi?', uko kwenye kibakuli kimezungukwa na milima. Kubwa zaidi, hapa tumesoma na vikoroboi; umeme mara upo, mara haupo. Na ikinyesha mvua, yale manyunyu ya awali, umeme unakatwa, maji

pia yanakatwa. Tulikuwa tunashuka na ndoo kwenda kwa walimu kule chini kutafuta maji, na kule kama hayapo tunashuka kwa wananchi kutafuta maji. Ninataka niwaambie tulikuwa tunachota maji tunaweka chumbani, kuna kitu kinaitwa *shabu* unaweka usiku, ukiamka asubuhi, maji yamejichuja, unatoa lile povu la juu unachuja yale masafi na kuyaweka kwenye chupa ya maji  kwa ajili ya kunywa, mengine yanakuwa ya kuoga. Hali ilikuwa hiyo, lakini tulisoma, tulifinyangwa, tumekuwa hivi tulivyokuwa.

Sasa ninyi wanafunzi mnaosoma leo na raha zote hizi, hamna sababu ya kutosoma vizuri. Kama sisi na shida zote tulisoma vizuri, hamna sababu kwa nini na nyinyi leo msisome vizuri.

Profesa Mwegoha endelea na jitihada zako za *crowdfounding*, Wanamzumbe tupo, tukakuunga mkono, na mimi ningependekeza tuanze na lile la mabweni ya wasichana. Mimi nitakagua mfuko kuona tutachangia kiasi gani kupitia kwa Profesa Adolf Mkenda, na wenzangu Mheshimiwa Emmanuel Nchimbi, Mheshimiwa Pindi Chana, Mheshimiwa Ashatu Kijaji, na wenyewe wachangie ili tuwajengee mabweni wenzetu kule Mbeya.

***Mheshimiwa Mkuu wa Chuo*;** nimezisikia baadhi ya changamoto nyingine, ila nimaani Prof Mkenda anaweza kuzitatua, na pale atakapozidiwa mtatufuata mtuambie ili tuweze kusaidiana. Kwa upande mwingine, katika dhamira yetu ya kuendelea kushirikiana na vyuo na taasisi za elimu ya juu, kama Serikali tunashughulikia changamoto kadhaa kama ilivyotajwa vizuri na Profesa Binamungu. Lakini niseme kwamba tutaongeza uwekezaji katika teknolojia, tafiti zenye manufaa, na mipango yenye lengo la kuimarisha elimu ya juu na kuwezesha wahitimu kuwa na ushindani kikanda na kimataifa. Tutaendelea kutafuta fedha kuwekeza kwenye maeneo hayo na tuendelee kuboresha elimu yetu na kujibu changamoto za mazingira ya sasa, kitaifa, kikanda na kimataifa.

***Mheshimiwa Mkuu wa Chuo***, ninapohitimisha, niruhusu niushukuru tena uongozi wa Chuo kwa kuniingiza kwenye historia ya Chuo hiki chenye heshima kubwa. Ninaipokea heshima hii kwa unyenyekevu mkubwa sana, na imeniongezea chachu ya kuongeza bidii kuwahudumia wananchi wenzangu.

Kwa wahitimu wenzangu, hongereni sana kwa juhudi zenu na kwa mafanikio haya. Kumbukeni kuwa, mmejifunza kwa maendeleo ya watu, mmejifunza ili mkafanya maendeleo ya watu. Elimu mliyoipata hapa, ikawe daraja kati yenu na wananchi, badala ya kuwa ukuta wa kuwatenga na jamii yenu.

Nihitimishe kwa kukumbusha tena lile ombi kwa Makamu Mkuu wa Chuo. Nilisema chuo hiki kilianzishwa kwa madhumuni ya kunoa viongozi kama tanuru la kuoka viongozi. Lakini kutokana na maendeleo ya elimu katika nchi yetu, chuo kimekuwa kama vyuo vingine. Niombe sana tusiache jukumu lile ambalo tulianzishiwa, la kulea viongozi wetu. Tunateua Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Mikoa, Mawaziri na Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu; wote wanatakiwa kupata msasa, wanataka kupata mambo mapya ili waweze kutuongoza vizuri. Niombe sana jukumu lile tusilitupe mbali, twende nalo, na kama tulivyokubaliana mara ya mwisho nilivyofika hapa, mliniambia mipango ipo mbioni, niwaombe muendelee, na mkikwama kupitia kwa Waziri njoo tuonane, tuzungumze, tujue tutamega wapi ili tuwe na eneo maalum la kunoa viongozi wetu.

Baada ya kusema hayo niseme asanteni sana kwa heshima hii.

Asanteni kwa kunisikiliza.

**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!**